

Mustakabali usiokuwa na sumu ni muhimu kwa maendeleo endelevu

Agosti 2018

Tukiwa asasi za kiraia (AZAKI) zinazotetea maslahi ya jamii, tunajiunga katika kampeni ya kimataifa kwa mustakabali (siku za baadaye) usiokuwa na sumu kama sehemu ya urithi wa maendeleo endelevu. Maono yetu ni kuwa na dunia ambayo kemikali na taka haziwi tena chanzo cha madhara na ni mahali ambapo watu wote wana haki ya mazingira salama na safi, yasiyo na tishio la sumu kwa mazingira yanayoizunguka na kwa vizazi vijavyo.

Tuta:

1. Tumia kanuni ya tahadhari na kutoa kipaumbele kwa kutumia taratibu za kinga (Kanuni ya Rio 15)
2. Toa umuhimu kwa ushirikishwaji sawa wa wanawake katika kufanya maamuzi, kufanya kazi ya kukusanya taarifa katika mchanganuo wa jinsia, na kukuza sera zinazowalinda wanawake kutoptana na kemikali na taka zenyne madhara. (SDG5)
3. Tetea uwepo wa maslahi mazuri ya watoto wakati wa uandaaji na utekelezaji wa sheria za afya ya jamii, mazingira na kazi ili kuwalinda watoto kutoptana na sumu na uchafu. (SDG 3, Haki za Mtoto)
4. Fanya kazi ili kusitisha uzalishaji na matumizi ya viuutilifu vya kemikali, hasa viuutilifu vyenye madhara makubwa na kuandaa programu za kitaifa za kukuza na kutekeleza kilimo ikolojia ili kuimarishe kilimo endelevu. (SDG 2)
5. Fichua uchafuzi na kemikali katika bidhaa na mifumo ya uzalishaji na kutetea na kutekeleza haki ya kupata taarifa kuhusu uingiaji wa kemikali na taka na kutoa taarifa kamili ya uwepo wake katika bidhaa. (SDG 12. Kanuni ya Rio 10)
6. Tambua, ainisha na tetea usafishaji wa maeneo yaliyochafuliwa na sumu ikiwa ni pamoja ushirikishwaji wa kina wa jamii na kuhakikisha usawa kati ya vizazi na kukuza urejeshaji wa ikolojia. (SDG 15)
7. Kukuza uelewa wa jamii kuhusu kemikali na taka zenyne madhara ikijumuisha upimaji wa hewa, ardhi, maji, chakula, bidhaa na watu na kukuza uandaaji na utekelezaji wa mifumo salama na mibadala, ikiwepo mibadala isiyokuwa na kemikali, na kuimarishe sheria za kupunguza na kuzuia uchafuzi. (SDG 6, 12,16)
8. Fanya kazi kupunguza na kuondoa uchafu baharini ikijumuisha zebaki, uchafu wa kiongani unaodumu muda mrefu katika mazingira, kemikali zinazoharibu mfumo wa homoni (*endocrine*) na plastiki.
9. Fanya uhakiki wa taka, kukuza urejelezaji na kuopuka uzalizaji taka, na kuhimiza sera za taka kuwa malighafi bila kurejeleza taka zenyne kemikali za sumu kuwa bidhaa mpya. (SDG 11)
10. Tetea na kutekeleza sera za afya na usalama mahala pa kazi zinazotoha haki stahiki ya kufahamu, kutoa kipaumbele kuzuia na tahadhari, kuandaa viwango ukomo vya kulinda walio katika hatari zaidi na kutoa kinga sawa mahala pa kazi na katika jamii.(SDG 8, 9)
11. Fanya kazi na serikali ili kusitisha vifungashio vya plastiki na bidhaa za plastiki zinazotumika mara moja tu na madini ya risasi katika rangi, vanishi, enamel, *glazes*, *primer*, na vitu vingine vya kupaka. (SDG 3, 12, 14)
12. Shiriki kikamilifu katika kufanya maamuzi na kutekeleza sera na makubaliano katika ngazi za taifa, kanda (kibara) na dunia kuhusu kemikali na taka (SDG 16, Kanuni ya Rio 10)
13. Kuzitaka sekta binafsi kuzingatia Miongozo na Kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu; kuwajibika kubeba gharama zote za uzalishaji wa kemikali ikiwepo miundombinu ya taka na urejelezaji; kuzitaka zikubali kuwajibika na bidhaa zao na matokeo yake hata baada ya uzalishaji; zitoe taarifa ili yokamilika ya usumu wa kemikali ikiwepo *nanomaterials* (chembechembe ndogo sana zinazotumika kuzalisha bidhaa); kutoruhusu kemikali na taka za sumu kuingia katika mazingira; na

kutekeleza kemia ya kijani katika kuzalisha bidhaa ambazo hazina sumu, zinazodumu na zinaweza kutumika zaidi ya mara moja. (SDG 8,9,12, 17, Kanuni ya Rio 16)